


# Ofisi ya AG na ndoto ya kuwa chachu ya kufikia malengo ya Dira 2050

**NA MWANDISHI WETU**

MALENGO ya Dira ya Taifa 2050 inalenga kuwa na Utumishi wa umma unaowajibika, hivyo matarajio ni kuwa na utumishi wa umma unaofanya kazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa.

Dira hiyo ni ndoto ya Ofisi ya Mkuu wa Serikali katika kuona haya yote yanafikiwa.

Akizungumza namna ya kufikia lengo hilo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza S. Johari, amesema kuwa Ofisi yake imejipanga kufanya maboresho katika Sheria mbalimbali ili kuweza kufikia malengo hayo ya Dira 2050.

"Tutahakikisha kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakuwa chachu ya kufikia malengo ya Dira 2050, inalenga kuwa na Utumishi wa umma unaowajibika, hivyo Matarajio ni kuwa na Utumishi wa Umma unaofanyakazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa.

Ni dhahiri kuwa kuwa Mabaraza ya wafanyakazi kwetu ni nyenzo muhimu kwa ustawi wa watumishi, taasisi na Taifa katika kufikia malengo ya DIRA 2050."Anasema.

Katika kukamilisha hilo, serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amewawezesha kwa Rasilimali na vitendea kazi mbalimbali vinavyowawezesha Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza Majukumu yao kwa urahisi.

Hivyo Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni jukumu lao kutumia vema muda wa kazi kwa kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi, ili kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria, kupitia utoaji wa huduma za kisheria kwa ubora unaotakiwa na ufanisi na tija inayotarajiwa kwa wadau mbalimbali.

Pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeeleza mafanikio yake kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 2,324 ilifanyiwa upekuzi kati ya mikataba 2,000 iliyokuwa imepangwa kufanyiwa upekuzi ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16 ya utekelezaji.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kufanya upekuzi wa Hati za Makubaliano (Memorandum of Understanding) 396 kati ya 600 iliyokuwa imepangwa ambapo ni sawa na asilimia 66 ya utekelezaji.



Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi na ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara, huduma za kitaalam, na ununuzi wa bidhaa.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya maombi ya ushauri 1,897 kutoka kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na wadau wengine.

Ofisi hiyo imefanikiwa kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya kwa kuzindua na kuendesha Kliniki bure za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa ya Manyara, Simiyu na Dar es Salaam na Wilaya zake.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuunganisha Mfumo wa OAG-MIS na Mifumo ya Kesi (Case Management Systems) ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Tanzania.

Kwa upande wa Wafanyakazi Serikali imeboresha mazingira na maslahi ya Watumishi, yanayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika kukamilisha Dira 2050, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa karibu na Mahakama kutokana na kutambua mchango mkubwa inayotoa katika jukumu la utoaji haki nchini ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kutekeleza wajibu huo, Mawakili wamekuwa kiungo muhimu baina ya wananchi na Mahakama katika kuichambua na kuitafsiri haki na sheria. Hivyo Mawakili wana nafasi kubwa katika kuhakikisha jukumu la utoaji haki linatekelezwa kwa ufanisi na Mahakama.

Wakiwa wao ndio maofisa wa Mahakama wamekuwa wakisaidia Mahakama kutekeleza jukumu la utoaji haki nchini kwa kutoa tafsiri sahihi za sheria ili kuisaidia Mahakama itende haki na kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki zao wanapokwenda Mahakamani au kwenye vyombo vingine vya kisheria.

Jambo hili halifanyiki pale shauri linapokuwa linaendelea pekee bali hata wakati wa utekelezaji wa hukumu.

Haya yote yamekuwa yakifanywa katika harakati za kusimamia haki, kwa kuwa wanatambua jukumu lao ni kubwa zaidi ya kuwawakilisha wateja kutokana na kuwa walinzi wa haki.

Katika kutekeleza Dira 2050 katika utoaji wa haki, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imekuwa ikiendesha Kliniki za msaada wa kisheria katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mwaka 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianzisha Kamati za Ushauri wa Kisheria katika ngazi za mikoa na Wilaya ili kurahisisha ufikiwaji wa huduma za ushauri wa kisheria kwa wananchi.

Miongoni mwa majukumu ya Kamati hizo ni kusaidia wananchi kupata haki zao mahali ambako haki hizo zinaweza kupatikana ili kupunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya Serikali na kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta haki zao.